

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 17.11.2021 HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA

1.0 WAJUMBE WALIOHUDHURIA

- | | | |
|----|----------------------|------------|
| 1. | Bw. Babyus Mashauri | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Solomon Mwangosi | Katibu |
| 3. | Dr. Bandioti Gavyole | Mjumbe |
| 4. | Bw. Gregory Fabian | Mjumbe |
| 5. | Bw. Hamza Kambuga | Mjumbe |

1.1 WAALIKWA:

- | | | |
|----|------------------|----------------------------------|
| 1. | Jofrey Kamwava | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango |
| 2. | Bw. Daniel Mbaki | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |

1.2 SEKRETARIETI

- | | | |
|----|----------------|--------------------|
| 1. | Paschazia Paul | Mwandishi wa Vikao |
| 2. | Jerry Lukinga | Afisa Manunuzi |

2.0 MUHT.NA.70/2021: KUFUNGUA KIKAO

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao baada ya akidi kutimia.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuwataka wawe makini katika kujadili agenda hiyo muhimu iliyokuwa mbele yao.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 02:30 Asubuhi.

3.0 MUHT.NA.71/2021: KUTHIBITISHA AGENDA

Mwenyekiti aliwaomba wajumbe kupitia agenda, wajumbe walipitia agenda hizo na kuthibitisha kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Maombi ya matumizi ya fedha za UVIKO 19 kiasi cha Tshs. 1,790,000,000/= kwa njia ya force akaunti

4.0 Kufunga kikao.

4.0 **MUHT.NA.72/2021 MAOMBI YA MATUMIZI YA FEDHA ZA UVIKO 19 KIASI CHA TSHS. 1,790,000,000/= KWA NJIA YA FORCE AKAUNTI**

Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi aliwasilisha maombi ya matumizi ya fedha za UVIKO 19 kiasi cha Tshs. 1,790,000,000/= ili zitumike kwa njia ya force akaunti kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 85 ya Shule za Sekondari kwa gharama ya Tshs. 1,700,000,000/= na Ujenzi wa nyumba ya watumishi wa hospitali ya Wilaya (Three in One) kwa gharama ya Tshs. 90,000,000.


Kikao kilipokea taarifa hiyo kisha kuridhia kuwa utekelezaji wa miradi hiyo ufanyike kwa njia ya force akaunti kwa kuwa haya ni maelekezo ya Serikali.

5.0 **MUHT.NA.73/2021 KUFUNGA KIKAO**


Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa namna walivyojadili na kutaka waendeleo na moyo huo.

Alifunga kikao saa 5:14 Asubuhi.

MWENYEKITI.....


UMETHIBITISHWA NA;

KATIBU.....


TAREHE

.....17-11-2021.....